# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.28. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya July 1-10, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Julai 11-20, 2023*



**MUHTASARI**

- Maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa makavu na hali ya ubaridi kiasi
- Hali ya upepo wa wastani hadi mkali na mawimbi makubwa baharini inayotarajiwa inaweza kuathiri shughuli za uvuvi hususan kwa maeneo ya ukanda wa pwani
- Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini, wafugaji wanashauriwa kutumia maji na malisho yaliyopo kwa uangalifu


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2023


Katika kipindi hiki migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika na ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii iliendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo nchini na kuimarisha mwendokasi wa upepo katika mwambao wa pwani na kusafirisha hewa yenye ubaridi kuelekea baadhi ya maeneo ya nchi.

Kwa upande mwengine, joto la bahari ya Hindi lilikua la wastani katika eneo la mashariki na juu kidogo ya wastani hadi wastani kwa upande wa magharibi. Hali hii ilichangia katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya pwani.

Katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola), joto la bahari lilikua la juu kidogo ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2023

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalikuwa makavu kwa ujumla isipokuwa maeneo machache ya mikoa ya Morogoro, Njombe, Ruvuma, Manyara, Kilimajaro, Simiyu pamoja visiwa vya Unguja na Pemba ambayo yaliyopata mvua kati ya milimita 11 hadi 50 kama inavyoonekana katika kielelezo.




Kielelezo: Makadirio ya kiasi cha mvua kutokana na satelaiti katika kipindi cha Julai 1-10, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2023

Katika dikadi hii, zao la mahindi katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Kagera, Morogoro, Arusha na Pwani limeripotiwa kuwa katika hatua ya kukomaa. Zao la mpunga hususan katika mikoa ya Pwani na Morogoro liliendelea kukauka na wakulima katika maeneo mengi walikuwa wanamalizia shughuli za uvunaji wa zao hilo.

Kwa upande mwingine, baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka wakulima walikuwa wanajihusisha zaidi na uvunaji na uhifadhi wa mahindi na mpunga, isipokuwa kwa maeneo ya mikoa

wa Njombe ambako zao la mahindi lilikua katika hatua ya kukomaa na kukauka.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ulikuwa wa kawaida katika maeneo mengi nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 1-10, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kimepungua kiasi katika mabonde mengi nchini.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2023

Katika kipindi hiki migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo katika kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendele kuimarika. Hali hii inatazamiwa kuendelea kuimarisha ukanda wa mgandamizo mkubwa wa hewa katika baadhi ya maeneo nchini na hivyo kusababisha kuendelea kwa vipindi vya upepo mkali katika maeneo ya ukanda wa pwani.

Joto la bahari katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola), magharibi mwa bahari ya Hindi na eneo la kati la Ikweta ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani.

Kwa upande mwengine, joto la baharí mashariki mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa chini kidogo ya wastani. Hali hii kwa ujumla inatarajiwa kuwa na mchango kidogo katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya pwani na kutokuwa na mchango katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2023

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla ikiambatana na vipindi vichache vya ngurumo za radi.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa na vipindi vifupi vya vya mvua nyepesi yenye upepo wa wastani hadi mkali na mawimbi makubwa baharini.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yakiambatana na hali ya ubaridi.

Maeneo ya pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla yenye upepo wa wastani hadi mkali na mawimbi makubwa baharini vinatarajiwa.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2023

Hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika maeneno mengi ya nchi itasaidia katika kukomaa kwa mahindi pamoja na shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mavuno zinazoendelea. Aidha, hali ya baridi inayotarajiwa katika maeneo mbalimbali nchini inaweza kuathiri ukomaaji wa mazao na afya ya mifugo.

Hali ya upepo wa wastani hadi mkali na mawimbi makubwa baharini inayotarajiwa inaweza kuathiri shughuli za uvuvi hususan kwa maeneo ya ukanda wa pwani. Hata hivyo jamii za wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye baharini ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini, wafugaji wanashauriwa kutumia maji na malisho yaliyopo kwa uangalifu.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 11-20, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kinatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na hali ya ukavu na upepo inayotarajiwa katika maeneo mengi.

Jamii inashauriwa kuendelea kutumia maji yaliyopo kwa uangalifu kufuatia kuendelea kwa msimu wa ukavu na baridi katika maeneo mengi nchini.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)